

**Na Sultan HAJIYEV,**
Balozi wa Jamhuri ya Azerbaijan nchini Kenya na Kongo-Brazzaville,
Mwakilishi wa Kudumu wa Jamhuri ya Azerbaijan katika Ofisi ya
Umoja wa Mataifa ya Nairobi


# Azerbaijan-Kenya: Mbali kwa masafa ila karibu zaidi

**Wasomaji Wapendwa,**

Tuna furaha kubwa kuwaletea toleo la kwanza kabisa la Kiswahili la Jarida la IRS, linalolenga kuwafahamisha hali halisi, mafanikio na michango ya Jamhuri ya Azerbaijan kimataifa. Chapisho hili linalenga kuwafahamisha na kuwavutia si tu marafiki zetu Wakenya lakini pia zaidi ya wazungumzaji milioni 200 wa Kiswahili barani Afrika, kwa kukuza ufahamu na uhamasisho mkubwa wa hadithi ya kuvutia ya Azerbaijan.


Afrika ni bara lenye fursa na ushirikiano mwingi na haya ndiyo hasa yanayolifanya kuwa moja ya vipaumbele vya juu vya Azerbaijan. Kupitia mahusiano yetu endelevu na Jamhuri ya Kenya, tunadumisha ushirikiano mkubwa katika sekta mbalimbali zinazovutia pande zote.

Mwaka wa 2024, tulisherehekea Maadhimisho ya Miaka 20 ya mahusiano ya kidiplomasia kati ya Azerbaijan na Kenya, yaliyoanzishwa tarehe 28 Mei 2004



– hatua inayoonyesha kuaminiana na urafiki uliojengwa kwa miongo miwili.

Mahusiano ya kirafiki kati ya viongozi wetu yanaendelea kuimarisha ushirikiano huu, hasa mkutano uliofanyika kati ya Mheshimiwa Rais Ilham Aliyev na Mheshimiwa Rais William Ruto tarehe 23 Septemba 2024, katika Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa huko New York.





Ubalozi wa Azerbaijan ulioko Nairobi, ulioanzishwa katika majira ya kiangazi ya 2023, umefungua ukurasa mpya katika mahusiano yetu. Tunajivunia hatua dhahiri tulizopiga pamoja na wenzetu Wakenya katika kuimarisha ushirikiano na kutambua njia mpya za kushirikiana kwa manufaa ya mataifa yetu mawili. Ubalozi huo unapoanza kufanya kazi kikamilifu, zikiwemo huduma za kibalozi, Wakenya sasa wana fursa ya kusafiri kwenda Azerbaijan na kuimarisha mahusiano kati ya wahusika.

Mwezi Machi, 2023, Waziri Mkuu wa Baraza la Mawaziri wa Kenya na Waziri wa Masuala ya Kigeni, Mheshimiwa Musalia Mudavadi, alihudhuria Mkutano






wa NAM Contact Group kuhusu Kukabili Ugonjwa wa COVID-19 huko Baku. Baadaye alishiriki katika Mkutano wa Viongozi wa Dunia wa Kukabili Mabadiliko ya Tabianchi katika COP29, uliofanyika Azerbaijan mnamo Novemba 2024.

Mnamo Juni 2025, Waziri wa Masuala ya Kigeni wa Azerbaijan, Mheshimiwa Jeyhun Bayramov, alifanya ziara rasmi nchini Kenya, ambapo alipokelewa na Mheshimiwa Rais William Samoei Ruto na kukutana na maafisa wengine wakuu.

Nchi zetu mbili zimeanzisha ushirikiano kupitia Mkataba wa Maelewano kuhusu Mashauriano ya Kisiasa, uliotiwa saini huko New York mnamo Septemba 2024, na raundi ya kwanza ilifanyika huko Nairobi mnamo Mei 2025.

Tunajivunia pia kuwa Kenya ni miongoni mwa nchi 60 zilizo na sura ya kitaifa ya Shirika la Vijana la Vuguvugu Lisiloegemea Mrengo Wowote (NAM, Non-Aligned Movement), lililozinduliwa kwenye mpango huu wa Mheshimiwa Rais Ilham Aliyev.

Ushirikiano wa kielimu na vijana ni nguzo kuu ya utangamano wetu. Tangu 2024, wanafunzi Wakenya wamenufaika kutokana na Mpango wa Kimataifa wa Ruzuku ya Elimu wa Heydar Aliyev, mpango unaofungua fursa mpya za ushirikiano wa kielimu na kitamaduni kati ya mataifa yetu. Hivi karibuni, Chuo Kikuu cha ADA cha Azerbaijan na Chuo cha Huduma za Kigeni cha Wizara ya Masuala ya Kigeni ya Jamhuri ya Kenya vimetia saini Mkataba wa Maelewano.






Kenya na Azerbaijan zina vipaumbele vinavyofanana katika kukuza nyumba za kudumu na maendeleo ya miji, juhudi zinazokubalika kimaeneo na kimataifa. Mpango wa Kenya wa kipekee wa Nyumba za Bei Nafuu unajitokeza kama mfano kwa Afrika na kwingineko, ukionyesha ahadi ya Serikali ya kuhakikisha hali bora za maisha kwa wote. Vilevile, baada ya kurejesha maeneo yaliyokua yamenyakuliwa, Serikali ya Azerbaijan imeanzisha mpango wa aina yake wa ukarabati, kujenga upya na kujumuisha maeneo yaliyoathiriwa na mgogoro huo. Ndani ya mfumo wa Mpango wa Taifa wa Marejesho Makuu ya Maeneo ya Jamhuri ya Azerbaijan, dhana bunifu kama vile «miji mahiri» na «vijiji mahiri» zinaanzishwa ili kukuza maendeleo ya kudumu na viwango vya maisha ya kisasa.

Si sadfa kwamba kikao cha kumi na tatu cha Kongamano la Miji Duniani (World Urban Forum, WUF13) kilifanyika huko Baku, Azerbaijan, kuanzia tarehe 17 hadi 22 Mei 2026, na mada yake ikiwa “Nyumba kwa Wote (Housing the World): Jamii na Miji Salama na Thabiti (Safe and Resilient Cities and Communities).» Kongamano hilo liliangazia kimataifa hitaji la dharura la kushughulikia changamoto ya nyumba na kubaini nyumba kama kichocheo kikuu cha maendeleo jumuishi, kakamavu na ya kudumu katika miji. Tukio hili lilileta jukwaa muhimu la mazungumzo na ushirikiano kati ya wadau wa miji ya Afrika na wa kimataifa.

Azerbaijan na Kenya zinapoendelea kupanua ushirikiano wake, nina imani kwamba urafiki wetu utaleta manufaa pande zote na fursa mpya kwa watu wetu. Ninawaalika wasomaji wetu Wakenya na wanaozungumza Kiswahili wasome toleo hili la Jarida la IRS ili watambue mada nyingi za Azerbaijani - taifa linalounganisha Mashariki na Magharibi, desturi na uvumbuzi, na lililojitolea kuhakikisha mustakabali wa kudumu.

**Sağ olun! Asante Sana!**





